
# NANI ATANIOKOLA ?

Siku ya Bwana moya nilikuwa nikihubiri Habari Njema katika mungini mukubwa wa sultani mumoya kwa inchi ya Basuto. Watu wingi walikutana kusikia Neno la Mungu, hata sultani vilevile pamoya na muke wake. Neno la Mungu lenye uwezo, lililo hai na kali kuliko upanga unaokata ngambo mbili, lilitobola roho za watu.

Wakati nilipokuwa nikihubiri, muke wa kwanza wa yule sultani mukubwa, ndiye malkia, alianza kutoa machozi na uchungu sana. Akasimama, akalalamika na taabu kubwa, **"Nani atakayeniokola?** Tafazali unisaidie, kwani moyo wangu una huzuni nyingi, niko mutu wa taabu kabisa. **Nani anayeweza kunisaidia? Nani atakayenifungula toka utumwa huu mubaya wa mauti?** Inanipasa kufanya nini? Ninyi wote munaniyua. Niko muke wa sultani na niko vilevile mumoya wa wanawake wa malombi. Kwa miaka kuliko makumi mbili ninakwisha kufika kwa nyumba ya Mungu, lakini maneno haya yote hayakunisaidia, hayawezi kuniokola, kwani zambi inakwisha kunifunga kabisa kabisa. Niko mulevi na niko mwuaji vilevile. Mikono yangu ni michafu na miovu kwa sababu inatumika nguvu kufanya pombe, kile kinyweo kinacholaa niwa. Zambi inakwisha kufunga migulu yangu na mikono yanguniko mufungwa wa Hadeze."



Akaketi tena, akalia na uchungu sana, "Munisaidie! Munisaidie! Nani atakayeniokola? Nani atakayenifungula katika vifungo vya zambi? Ninapenda Mungu, lakini zambi inanitawala na kunikokota chini hata Hadeze. Niliua mutoto wangu mupendwa, muzaliwa wa kwanza. Nililewa wakati nilipomubeba yulu ya mugongo wangu, na kwa sababu nilelewa nilifingirisha mwili wangu yulu ya udongo na kuvunja kichwa cha mututo naye alikufa. Munisaidie, muniokole toka mauti hii! Wachawi hawawezi kunisaidia. Dini haiwezi kunisaidia vilevile. Basi nani ataweza kunisaidia? Nani ataweza kuniokola?"

Nikamujibu nikisema, Salama iwe kwako. Watu wote wana taabu kama wewe. Kitabu cha Mungu, Biblia, kinaonesha jibu kwa kilio cha roho yako. Katika WaRoma 7:15-25 tunaona namuna zambi inavyotutawala na ni nani anayeweza kutuokola. Kwani ninayua ya kuwa ndani yangu, maana ndani ya mwili wangu, haliikali neno jema; ninataka kutenda yaliyo mema lakini ninakosa uwezo kuyatenda. Na mema ninayotaka kutenda, siyatendi, lakini mabaya ninayoyachukia na nisiyotaka kufanya, ninayafanya. Zambi inayoikala ndani yangu inanilazimisha wakati wote kutenda mabaya, na matendo mema ninayotaka kutenda siyatendi. Ninafurahia sheria ya Mungu kwa mutu wa ndani, lakini ndani ya viungo vyangu ninaona sheria nyingine ikipiga vita na ile sheria ya akili zangu, ikinifunga kama mutumwa wa sheria ya zambi iliyo katika viungo vyangu.

Siku nyingine kila mutu atalalamika, **"Ole kwangu mimi mutu wa taabu! Nani atakayeniokola!"** Kama tukilia kwa Mungu, Yeye atatujibu na kutuokola.

**JIBU**


*"Kama mwana basi anawaweka ninyi huru, mutakuwa huru kweli."*
*(Yoane 8:36).*

Yesu ni jibu la maulizo yetu yote. Ni jibu la ulizo lako. "Hakuna wokovu katika mungine, kwa maana hakuna jina lingine chini ya mbingu walilopewa watu tupate kuokolewa nalo." (Matendo 4:12). Yesu tu anaweza kutuokola toka zambi zetu. Damu Yake tu aliyoimwanga yulu ya musalaba inaweza kutusafisha toka zambi yote. Hakuna munganga wala muchawi, wala muhubiri, wala padre, wala mutu ye yote mungine, wala kanisa anayeweza kukuokola toka zambi. Yesu tu, Mwana-Kondolo ya Mungu anayeondola zambi ya ulimwengu anaweza kukuokola kwa damu Yake na kwa uwezo wa Roho Mutakatifu.

Yesu, Mwana wa Mungu, alikuya duniani kufungula macho ya vipofu, kufungula wafungwa toka munyororo na wale wanaoketi katika giza toka nyumba ya kufungwa. (Isaya 42:6,7). Yesu alisema kila mutu anayefanya

zambi ni mutumwa wa zambi na wa Satani, lakini kama Mwana (wa Mungu) akiwaweka ninyi huru, mutakuwa huru kweli. (Yoane 8:34-36). Yesu ndiye kweli ya Mungu inayotufungula toka utumwa.

Yesu, Mwana wa Mungu, alibeba zambi zetu zote katika mwili Wake yulu ya musalaba. Zambi zako zote zilifungwa kwa musalaba. Kweli amechukua taabu zetu, na amebeba huzuni zetu; azabu ya salama yetu ilikuwa yulu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona. (Isaya 53:3-7).



*"Kama mwana basi anawaweka ninyi huru, mutakuwa huru kweli."*
*(Yoane 8:36).*

Baraba alikuwa mwenye zambi kabisa, mwuaji, na alihukumiwa kufa. Ilimupasa kusulibishwa, lakini Yesu alimukombola, akabeba musalaba iliopasa Baraba kufa yulu yake. Yesu, Mwana wa Mungu, alisulibishwa kwa pahali pa Baraba, kwa pahali pako na kwa pahali pangu, na yule mwuaji alifunguliwa kwa sababu Mungine alikufa kwa pahali pake.

Wewe na mimini kama Baraba. Mushahara wa zambi ni mauti, lakini zawadi ya Mungu ni uzima wa milele katika Yesu Kristo. Kama ukitazama musalaba wa Kristo kwa imani, utaweza kuyiona mwenyewe pale ukifungwa kwa musalaba ule pamoya na zambi zako. Yesu anakwisha kukukombola ili uweze kuishi kwa milele kwa sababu ya damu ya Yesu iliyomwangika kwa musalaba kwa usamehe wa zambi zako. Kwani Mungu alikupenda sana hata alitoa Mwana Wake muzaliwa pekee ili usihitaji kupotea lakini uweze

kupata uzima wa milele.

Wakati muke wa sultani aliposikia maneno haya yote aliamini Yesu kabisa na kumutolea roho yake, Yeye aliyemukufilia yulu ya musalaba na kumwanga damu Yake ya damani kusafisha moyo wake toka zambi zote. Akamupa Mungu moyo wake wa zambi na Mungu alimupa moyo mupya na kumuyalisha na Roho Mutakatifu. Alimusamehe zambi zake zote, na tena alimwokola toka uwezo na utawala wa zambi. Kwa miaka mingi sasa tangu siku ile anaishi kwa utakatifu na anashinda zambi na kutukuza Mungu katika maisha yake. Hakunywi pombe kata kidogo wala kutumia tumbako, lakini anashuhudia kweli ya Mungu ya kuwa yeye aliye ndani ya Yesu Kristo ni kiumbe kipya. "Maneno ya zamani yamepita; tazama maneno yote yamekuwa mapya." (2 WaKorinto 5:17).

Wewe vilevile, musomayi mupenzi, unaweza kuokolewa kwa njia ya imani ku Yesu Kristo. Yesu alisema, "Kuyeni kwangu, ninyi **WOTE** munaosumbuka na wenye muzigo muzito, nami nitawapumzisha ninyi." Fika karibu na Yesu sasa. Umwambie wazi habari za zambi zako na masumbuko yako. Hatakufukuza kama ukikuya na roho ya toba na unyenyekevu na imani. Labuda wewe ni mutu wa kanisa tangu siku nyingi, lakini hata hivi zambi inakufunga. Kuya ku Yesu, naye atakufungula toka utumwa wa zambi mara moya, kama alivyoponesha mukoma na kufungula macho ya kipofu. Yesu hageuki, Yeye ni sawasawa leo kama alivyokuwa zamani na anaponesha mioyo ya kuvunjika na kufungula watumwa wa zambi. Anasamehe zambi zetu **ZOTE** na kuponesha magonjwa yetu **YOTE**. (Zaburi 103:3).

Wakati unapokwisha kupokea Yesu kama Mwokozi wako, ututumie barua. Tutapenda kukulombea. Labuda tutaweza kukusaidia na kukuongoza katika njia ya Mungu.

---

Si vous avez trouvé le salut en Christ ou si vous avez été béni par notre littérature, nous vous prions de nous le faire savoir. Nous aimerions remercier Dieu avec vous et prier pour vous.

**Notre Livre du Coeur est maintenant aussi disponible sur votre Téléphone cellular, plaques, etc. de www.angp-hb.co.za ou comme une Application "Heart of Man" sur téléphones Android.**

Pour obtenir gratuitement de la littérature évangélique, des livres et des traités en plus de 540 langues, écrivez à:

**E-MAIL: info@angp.co.za**

**ALL NATIONS GOSPEL PUBLISHERS**

**P.O. BOX 2191, PRETORIA, 0001, R.S.A.**

(Une Mission de Littérature évangélique financée de dons)

(Reg. No. 1961/001798/08)